

**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
20 Juni 2009**

Waliohudhuria

Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Ally Salum
Beda John Mkusu
Edgar R Paulo
Elaine Baker
Husein Hamza Hamisi
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Mejah Mbuya
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Selion Elieskia
Shamte J Kigoma
Shukuru Hassan
Sudi Saidi Ramadhan
Mbaraka Mohamed
Abdul Mwaibambe

Vitambulisho

Elaine alipiga picha kwa vitambulisho na atatengeneza vitambulisho kwa Mejah, Selion, Allan, Edgar, Abdul na Shamte.

Mkutano wa Tanga

Mejah alituonyesha picha za mkutano wa Tanga. Elaine ataweka repoti kwenye website. Kuna picha moja ya Dominata akimpa Meya wa Tanga, Bwana Kisauji, helmet na reflective jacket. Alisema alikutana na Professor Karonda wa Chuo cha Ardhi pia.

Mradi wa Wamba

Waalimu na washiriki kwenye mafunzo walisema kwamba yameenda vizuri. Diwani ya Manzese na Diwani wa Mkurumla walikuwa wageni rasmi. Wanafunzi 24 walihudhuria siku zote mbili.

Tulipiga mahesabu mengine lakini mahesabu mengine yatasubiri Filbert na Hamadi wawe kwenye mkutano. Pia wao wana fomu za maswali ya evaluation.

Allan alileta photo 8 za mafunzo. Elaine alilipa Tsh 8,000 kutoka kwa hela zake na itarudishiwa baadaye.

Helmets na jackets zinabaki kwa sababu ya kutokuwa na wanafunzi sitini. Hamadi Bwaja alichukua helmet moja.

Tulizidi badjeti ya watu 24 kwa sababu ya kupanga kuwa na watu 60.

Jumatatu tulipata contact ya mama moja anahitaji tutoe mafunzo shuleni karibu na nyumbani kwake Temeke.

Mafunzo ya kutoa mada

Jumatatu tulialikwa kwenye mafunzo ya vipi kutoa mada na NGO inayoitwa Mass Development Association, Temeke. Wanachama 13 walihudhuria.

Mkutano wa mashirika ya wapanda baisikeli, Nairobi

UWABA tumealikwa kwenye mkutano wa mashirika ya wapanda baisikeli, Nairobi. Mkutano ni tarehe 6 na tarehe 7 mwezi wa saba. Pia kuna msafara wa baisikeli tarehe 4, pia tumealikwa kushiriki.

Mkutano unaandaliwa na Interface for Cycling Expertise (ICE) wa Uholonzi pamoja na Uvumbuzi ambayo ni NGO huku Kenya. Kwanza walisema mtu mmoja ahudhurie na asafiri na ndege lakini Elaine aliomba watu zaidi wahudhurie na walikubali kwamba watu watatu wahudhurie wakisafiri na basi.

Tulifanya uchaguzi kuchagua watu kuhudhuria. Mejah Mbuya, Edgar Paulo na Filbert Mbecha walichaguliwa.

Elaine ataandaa vipeperushi. Atawauliza kuhusu lugha, meza ya maonyesho na maanadalizi mengine.

Mkutano wa usalama barabarani, Dar es Salaam

UWABA pia tumealikwa kwenye mkutano wa usalama barabarani hapa Dar es Salaam hoteli ya Kempinski. Jioni tarehe 7 mwezi wa saba kuna cocktail, tarehe 8 kuna mkutano wa hotuba, na Rais Kikwete anafunga rasmi na tarehe 9 na tarehe 10 kuna workshop. Inaandaliwa na Commission for Global Road Safety na ni mkutano wa watu kutoka Afrika mzima – serikali pamoja na mashirika ya siyo ya kiserikali.

Waliojisajili kuhudhuria ni: Elaine Baker, Husein Hamza Hamisi, Juma Hassan Chibaya, Paulo Atibu Hatibu, Shukuru Hassan, Selion Elieskia, Ally Athuman Jumbe, Juma Ali Salehe Jongo, Abdul Mwaibambe, Ally Salum, Mejah Mbuya. Kama kuna nafasi za ziada: Hamadi Bwaja, Dominata Rwechungura, Sosthenes Amlima.

Elaine ataandaa vipeperushi. Atawauliza kuhusu lugha, meza ya maonyesho, mavazi na maanadalizi mengine.

Re-cycle

Hotuba ya badjeti ya waziri ya fedha imetangaza serikali wana mpango wa kufuta msamaha ya kodi kwa NGOs, lakini bado wabunge wanachangia mawazo, basi tutasubiri matokeo.

JICA

Jumatatu tarehe 1 mwezi wa juni UWABA tulikutana na JICA. Elaine aliandika dondoo za mkutano huu. Pia alifuatalia kwa kuwatumia nakala za barua za TANROADS kuhusu Kilwa Road.

Kongamano

Kwa sababu hata JICA hawapo tayari kulipa posho kwa kongamano, tuliongeana kuhusu hatua gani kuchukua sasa. Mejah alikuwa na wazo kwamba tuwasiliane na Uli Malsius kupata ushari wake, pia Bwana Mbogoro.

Ushirika wa Fasta Cycle courier

Bwana Bukuku alisema tukutane naye tarehe 5 mwezi wa saba.

Mkutano na waziri ya miundombinu

Adam Msinga bado hajashirikiana na Mejah kuandika repoti kuhusu mkutano wa Ubeljiji basi Mejah atafanya pekee yake, halafu atatafuta mkutano na waziri ya miundombinu.

Ruzuku ya Foundation for Civil Society

Juma alipeleka maombi yetu ya ruzuku. Elaine atafuatalia na email kuhakikisha wanashughulikia.

Msafara

Muda imefika kuandaa kwa msafara wa mwezi wa kumi. Elaine ataandika proposal. Mejah atawasiliana na Vodacom. Edgar na Mejah watawasiliana na UNEP.

Ride Planet Earth

Ride Planet Earth waliomba UWABA tufanye msafara mdogo wa baisikeli mwezi wa kumi na mbili wakati wa mazungumzo ya mabadalika ya hali ya hewa. Mejah atawasiliana na mashirika ya mazingira kuona kama watashiriki pia.

Wimbo

Mejah anaendelea kutayarisha CD cover.

Video

Juma alipeleka CD TANROADS makau makuu. Bado traffic police (Mejah), na Star TV na DART (Sosthenes). ITV walisema quality siyo nzuri kwa TV. Mejah na Elaine bado wanafuatalia na TBC.

Mambo ya hela na guta

Filbert alipata dharura hajahudhuria basi mambo ya hela tutaongea wiki ijayo.